

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

List of characters by scenes:

SCENE ONE : NINA, PATO AND TUBU AT THE RIVER

- **Nina (f, 40)**
- **Pato (f, 35)**
- **Tubu (f, 35)**

SCENE TWO : MITUMBA AND KAVESI MEET AT KAVESI'S FARM

- **Mitumba (m, 50)**
- **Kavesi (m, 45)**

SCENE THREE: MASAMBO AND HIS SONS AT THE RIVER BANK

- **Lawi (m, 20)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Gulu (m, 17)**

SCENE FOUR: LELA AND SHANI PREPARE FOR THE FARM

- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f, 17)**

Msimulizi

INTRO:

Nawasalimu nyote na karibuni katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako.

Hiki ni kipindi cha tatu katika hadithi inayoendelea, tukiangazia jinsi ya kutatua mizozo kwa kutumia njia za utamaduni wa kiAfrika. Je njia hizi zina umuhimu

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

wowote katika ulimwengu wa sasa? Kipindi kilichotupa kisogo, Masambo aliudhiwa sana na wanawe, Lawi na Gulu, walipokuja na ng’ombe wachache baada ya ng’ombe wengine kuibwa na wezi wa ng’ombe wa Kimbebe. Wakati wuwo huwo, Mitumba alimpa onyo Nina, mke wa Masambo, kuhusu masuala ya mto. Sasa leo kutatibuka yapi? Usibanduke katika redio yako, upate kujiza “**Kizazi cha kisasi**”. Tunatabaruku na Nina, Pato, na Tubu, wanawake watatu kutoka bonde la Kijani wakiwa mtoni.

SCENE ONE: NINA, PATO AND OTHER WOMEN AT THE RIVER

1. SFX: RIVER WATER RUNNING DOWNSTREAM

2. NINA: (calling out) Tubu! Pato! Subirini . Kuna jambo nataka kuwaeleza.

3. TUBU: (tired) Ni kuhusu nini Nina? Wajuwa sisi twaenda mbali kukuliko.

4. PATO: (also tired) Ni kweli, kila tukija kuchota maji huku mtoni ni lazima tuage familia zetu kama ambae twaenda safari ya mbali.

5. TUBU: Kwani ni nini, kama si safari hii.

6. NINA: Tubu na Pato, hili ni muhimu, tafadhalini nisikizeni.
(Pato and Tubu act as if placing some water pots down)

7. PATO: Sawa, enhe?

8. NINA: Nafikiri waume zetu wanafanya mipango.

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

9. TUBU: Hiyo ni kawaida yao. Siku zote wao wana mipango ya kando.

(Pato and Tubu laugh)

10. NINA: Hamunielewi. Nafikiri, waume wetu wanapanga kwenda vitani.

11. PATO: (**shocked**) Ndio sababu mume wangu jana alirudi nyumbani kuchelewa?

12. TUBU: (**more shock**) Hata wangu basi.

13. NINA: (**relaxed**) Wangu pia. Walikutana, na kama kawaida, hatujui kuliamuliwa nini. Lakustikisha zaidi, Lawi na Gulu, vijana wangu wawili, walinyang’anywa ng’ombe na wezi wa mifugo wa Kimbebe. Waliporudi, mumewangu Masambo aliwaingiza ndani na hao watatu walizungumza hadi usiku wa manane.

14. PATO: Na hukuruhusiwa kusikiliza.

15. TUBU: Wanawake hawaruhusiwi kusikiliza wanaume wakizungumza. Huo ndio utamaduni. Mila yetu.

16. PATO: (**protesting**) Hiyo si sawa! Kwanini tutwengwe, katika masuala yanayohusu uhai au vifo vyta waume na watoto wetu?

17. NINA: Ndio nikasema nawajulisha, nashuku mambo yameharibika. Jitayarisheni.

18. TUBU: (**worried**) Tutafanyaje tuzuie uhasama huu?
Munajuwa mzozo huu umeletwa na nini?

19. NINA: Kwanza nikidhani ni wale majirani zetu wa Koroma

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “ Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

hana bonde la Kijani, lakini baada ya tukio la wezi wa Kimbebe, sina uhakika.

20. PATO: Watu wa Koroma? Nafikiri tulitatua tofauti zetu kitambo sana.

21. TUBU: Pato, tumewahi kutatua tofauti zetu na makabila mengi, lakini kila kizazi kipyka kikija huja na mzozo mpya.

22. NINA: Ni kweli. Mume wangu na wavulana wangu daima wanazozana na familia ya Mitumba. Kila kukicha wanawalaumu kuwa wanawaibia ardhi, maji na Mungu ni shahidi yao.

23. PATO: (**malicious**) Lakini kweli ndivyo walivyo! Wezi na wavamizi!

24. TUBU: (**sarcastic**) Wewe washawahii kukuibia nini, Pato?

25. NINA: Ah rafiki zangu! Wacheni hizi lawama! Tutakacho ni kusitisha hii mizozo kabisa. Suluhisho la kudumu. Alafu sote tuishi kwa amani.

26. PATO: Suluhisho la kudumu? Amani? Nina, wafu peke yao ndiyo wenye amani, na hao pia ni lazima wawe walitenda mema walipokuwa hai. Sisi, wa Torube hatujawahipo kujuwa amani. Hayo ndiyo maisha yetu. Jicho kwa ji.....

27. TUBU: ... kwa jicho. Na jino kwa jino.

28. NINA: Nishasikia msemo huo, jicho kwa jicho lakini athari yake ni kuwa dunia nzima itapofuka. Mama wenzangu. Ni lazima tukomeshe umwagikaji wa damu

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

isiyo hatia. Fikirieni. Ni hayo. Acheni niwasaidie
kuwabandika maji vichwani mwenu.

(Nina acts out helping to put the water on Pato's and Tubu's heads)

29. MSIMULIZI: Nina alihofia. Ameona uhaini unaosababishwa na wapiganaji
wenye silaha. Wanawake wana jukumu gani, katika kutafuta suluhu?
Itawezekana kweli? Ikitazamiwa kuwa mila na desturi zimeutenga
ulimwengu wao? Hata hivyo, mbali na mtoni, Mitumba baada ya
kuchokozwa na familia ya Masambo, alienda kwa mkabila mwenzake,
Kavesi, kumshitakia.

SCENE TWO: MITUMBA AND KAVESI MEET AT KAVESI'S FARM

**30. SFX: SOMEONE CUTTING DOWN A TREE WITH AN AXE (splitting
firewood)**

31. MITUMBA: Kavesi!!!

32. SFX: CONTINOUS CUTTING OF A TREE WITH AN AXE

33. MITUMBA: Bwana Kavesi.(pats him on the back)

34. KAVESI: (Shrieeks out of fright) Aaaah Mitumba, usifanye tena
hivyo siku nyengine. Ningekugeukia na shoka je?

35. MITUMBA: Pole, sikunuia kukugutusha.

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

- 36. KAVESI:** **(Catching breath)** Ni sawa. Munaendeleaje? Binti zako?
- 37. MITUMBA:** Twashukuru. Tunaweza kuzungumza au muda si mzuri?
- 38. KAVESI:** Yanaweza kusubiri? Au ni ya dharura?
- 39. MITUMBA:** Nikuhusu familia ya Masambo.
- 40. KAVESI:** Basi hayo hayawezi kusubiri! Nipe sekunde moja..

41. SFX: AXE IS STUCK INTO A LOG

- 42. KAVESI:** Ndio, niambie, wamekufanya nini hao wasio kuwa na miji yao? Kazi kuzurura tu.
- 43. MITUMBA:** Nianzie wapi? Hmm natatizika. Unajuwa mimi hutumia maji ya ule mto kunyunyizia shamba langu.
- 44. KAVESI:** Ndio najua.
- 45. MITUMBA:** Sijui ni nani hasa. Lakini mmoja wa waMasambo huja mapema kuzuia yale maji ya ule mto yasiingie kwenye shamba langu ili mimea yangu isipate maji.
- 46. KAVESI:** **(Shocked)** Ati! Kwa muda gani sasa wamekufanya hivyo?
- 47. MITUMBA:** Kwa juma moja sasa. Kama wanatukejeli. wanaziba, tunazibua, wanaziba tena, tunazibua te..
- 48. KAVESI:** Kwa ufupi, hawataki maji yafike shambani kwako.
- 49. MITUMBA:** Ndio.

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

- 50. KAVESI:** Na hiyo inamaanisha wewe ukose chakula pamoja na watoto wako.
- 51. MITUMBA:** Ndio. Kama hakutanyesha.
- 52. KAVESI:** Mitumba, una haki kama wengine kutumia huo mto . njoo, twende kulipiza kisasi!
- 53. MITUMBA:** Lakini, Kavesi, Sijamaliza kukueleza.
- 54. KAVESI:** Uliyonieleza yanatosha! Wanataka kutumaliza. Hakuna jengine. Njoo! Twende.
- 55. MITUMBA:** Wapi?
- 56. KAVESI:** Kama wanazuia mimea yetu isipate maji, nasi tutaizuia mifugo yao kunywa maji pia.
- 57. MITUMBA:** Ngoja Kavesi! Utaizuia vipi? Hatuhitaji tahiruki zaidi?
- 58. KAVESI:** Wameyaanza wao. Tutamaliza sisi!
- 59. MSIMULIZI:** Cheche moja ya kiberiti huzua moto mkubwa. Kavesi aliandamana na Mitumba hadi mtoni na kukita milingoti mirefu sehemu ng'ombe wanapokunywia maji ikawa vigumu ng'ombe kuyafikia maji. Jioni yake, wakati Lawi, Gulu na Masambo walipowasili na mifugo iliyobakia....

SCENE THREE: MASAMBO AND HIS SONS AT THE RIVER BANK

60. SFX: COWS MOOING

- 61. GULU:** (**alarmed**) Baa!, Tazama hakupitiki kwenda mtoni! Kuna mtu amekita nguzo kutuzuia tusitumie mto.
- 62. MASAMBO:** (**utterly shocked**) Nani anazuia ng'ombe zangu zisinywe maji? Muna hakika tuko kwenye mto wetu?

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

63. LAWI: Ndio baba ni hapa. Huyu lazima awe ni Mitumba. Yani anatuzuia tusitumie mto wetu .

64. SFX: COWS MOO EVEN LOUDER

65. GULU: Tufanyeje na wanyama wana kiu?..

66. LAWI: Na njaa pia.

(Short pause)

67. MASAMBO: (**Supressed rage**) Ongozeni ng'ombe kwenye shamba la Mitumba! Waacheni wale mimea mpaka washibe, alafu, waacheni wanywe maji yayo hayo yanayokuja shambani kwake!

68. LAWI: (**unsure**) Ati.. Lakini..

69. MASAMBO: (**furious**) Hakuna cha lakini! Fanyeni nilivyosema. Ni wakati waKoroma, watujuwe sisi waTorube, ni kina nani.

70. GULU: (**leading cows**) ..Essh essssh..kule.. kule shambani!!!..esssssh!

71. SFX: COWS MOO, SHEEP AND GOATS BLEAT

72. MSIMULIZI: Masambo na wanawe waliwaongoza ng'ombe shambani kwa Mitumba, hapo ndipo ng'ombe walipopewa mualiko wa karamu kubwa, walikula kila aina ya mimea na nyasi zilizonawiri kwa kijani. Walikula wasibakishe kitu kama kwamba shamba ndio mwanzo lilikuwa limetayarishwa kuanza kupandwa sasa. Asubui iliyofuata, wakati Lela na

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

Shani kama kawaida yao walipokuja shambani kwa baba yao kufanya kazi.....

SCENE FOUR: LELA AND SHANI PREPARE FOR THE FARM

73. SFX: MORNING AMBIENCE IN THE VILLAGE

74. LELA: Shani usisahau kitu chochote.

75. SHANI: Mbona ni mimi kila siku nabeba vitu peke yangu?

76. LELA: (Laughs) kwa sababu wewe ni mdogo.

77. SHANI: Lela, wewe ni dhalimu! Mbona leo hatuandamani na baba? Sitaki kubaki peke yangu shambani.

78. LELA: Peke yako? Si mimi niko Shani. Baba anafuatilia mambo mengine. Atakuja baadae. Twende.

79. SFX: DOOR CLOSED AND LOCKED

80. SHANI: Lela, ati ni kweli watu wetu wakifa huwa wanaenda mbinguni kumwambia Mungu atuletee mvua?

81. LELA: Hivyo ndivyo baba aliniambia, na yeye aliambiwa na babake, na babake naye akaambiwa na babake....
Kila kizazi kinapokezwa ufahamu huo... .

82. SHANI: Kwa hivyo haya mawingu ni watu wetu wale wamekufa? Basi ni wengi.

83. LELA: Ndio, lakini sio watu wa Koroma pekee, hawa ni watu wa dunia nzima.

84. SHANI: (Totally alarmed) Lela, angalia shamba letu!

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

Kipindi cha 3: “Kizazi cha kisasi”

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

85. LELA: **(Devastated)** Oh la! Oh hapana. Mungu wangu
la!!!!!!

86. SHANI: **(weeps bitterly)** Hapana!!!!!!

OUTRO:

Vilio hivyo duni na dhaifu vyta Shani na Lela vikilihanikiza bonde la Kijani, tunahitimisha sehemu tatu ya hadithi hii ya mizozo na utatuzi. Jiunge nasi juma lijalo wakati wanaume wataingia vitani, Je kweli tutashuhudia vita vyta makabila haya mawili? Au suluhu itapatikana badala ya vifo na uharibifu unaoletwa na vita vyta silaha? Kwa haya na mengine zaidi, au kama unataka kusikiliza tena kipindi hiki, chengine kilichopita au kutuma maoni, basi tembelea tovuti yetu. www.dw.de/kiswahili

Mpaka tutakapokutana tena, dumisha amani!